JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

STASHAHADA YA UALIMU MWAKA WA PILI

MODULI ELEKEZI YA KISWAHILI

November 2007

© *WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI*

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuchapa au kutoa moduli hii kwa jinsi yoyote bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Imetayarishwa na:-
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S.L.P. 9121
DAR ES SALAAM
TANZANIA.

Tel: …….
Fax……
E-mail……..

YALIYOMO

Ukurasa

SHUKRANI..... iii

UTANGULIZI iii

NAMNA YA KUTUMIA MODULI v

1.0 UTUMIZI WA MSAMIATI NA MIUNDO YA KISWAHILI.....1

2.0 MATAMSHI NA LAFUDHI YA KISWAHILI.....7

3.0 FASIHI 9

4.0 UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI 12

5.0 MAENDELEO YA KISWAHILI 14

6.0 UFAHAMU 16

7.0 UANDISHI 20

8.0 SARUFI 23

ORODHA YA VITABU.....25

SHUKRANI

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inapenda kutoa shukrani za dhati kwa wataalamu walioshiriki katika kuunda na kuendeleza mwongozo huu.

Waandishi:

- Bibi Edith Mdoe - Chuo cha Ualimu Vikindu
- Bwana Said J. Kondo - Chuo cha Ualimu Korogwe

Waratibu

1. Samuel J. Makundi - Idara ya Ualimu
2. Naomi V. Swai - Idara ya Ualimu

Katibu Muhtasi:

Anna Hamis - Ofisi ya Afisaelimu Kiongozi

……

AFISA ELIMU KIONGOZI

UTANGULIZI

Moduli hii ni ya mafunzo ya Kiswahili kwa mwalimu mwanafunzi wa Stashahada mwaka wa pili aliyeko katika mazoezi kwa vitendo. Moduli hii ina mada nane.

Mada zote zimezingatia kumjengea Ujuzi mlengwa utakaomsaidia yeye mwenyewe kujijenga Kitaaluma na Kitaalamu. Baada ya kusoma mada zote mwalimu mwanafunzi anatarajiwa apate ujuzi ufuatao:-

1. Kuandika na kuzungumza Kiswahili kwa usahihi.
2. Kubaini, kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.
3. Kuhakiki kazi za fasihi simulizi na andishi kwa kuzingatia vigezo vya uhakiki.
4. Kutunga kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi.
5. Kubaini hatua mbalimbali za kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania na duniani kwa ujumla.

NAMNA YA KUTUMIA

Ili kufaidika barabara na moduli hii mwalimu mwanafunzi anatarajiwa asome vitabu vingine vilivyoainishwa mwisho wa moduli hii na vinginevyo ili kujijengea uwezo wa kufanya mazoezi yaliyoainishwa katika kila mada ndogondogo, kutunza kumbukumbu za kazi mbalimbali, ukusanyaji wa kazi za fasihi na kuzihifadhi pamoja na matumizi bora ya mkoba wa kazi.

Vilevile ni matarajio yetu kuwa mwalimu mwanafunzi ataitumia vyema moduhi hii ili kumjengea uwezo kitaaluma na kitaalamu, ili kumsaidia katika mtihani wake wa mwisho anaotarajia kuufanya baada ya kumaliza mazoezi kwa vitendo.

Ni matarajio yetu kuwa moduli hii itamjengea mwalimu mwanafunzi ujuzi uliobainishwa kwenye utangulizi wa moduli hii.

MADA YA KWANZA
UTUMIZI WA MSAMIATI NA MIUNDO YA KISWAHILI

1.1 Kutumia maneno ya Kiswahili kwa Usahihi.

Maudhui

Katika mada hii umejifunza aina za maneno kwa kutumia mawazo ya wanaisimu mbalimbali. Umejifunza pia jinsi ya kutumia maneno hayo ya Kiswahili katika mazingira tofauti. Sasa unapaswa kujikumbusha yafuatayo ili kujipima kitaaluma na kitaalamu.

Ujuzi

Baada ya kujifunza mada hii utaweza:

(a) Kufafanua aina za maneno ya Kiswahili

(b) Kutumia aina mbalimbali za maneno ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali.

Shughuli za Kufanya

1. Kwa kutumia mawazo ya wataalamu mbalimbali jadili aina za maneno ya Kiswahili.
2. Kwa kutumia mifano dhahiri eleza jinsi utakavyomsaidia mwanafunzi Kutofautisha
   (a) Kiwakilishi na kivumishi
   (b) Kiunganishi na kielezi.
3. Andaa somo la dakika 80 ukionyesha namna utakavyofundisha aina za maneno ya Kiswahili.
4. Fundisha somo hilo na bainisha yafuatayo:
   (a) Wanafunzi wenye matatizo katika kutofautisha kiwakilishi na kivumishi, kiunganishi na kielezi
5. Bainisha mbinu utakayotumia kuwasaidia wanafunzi hawa kupata dhana hizi kwa uhalisia na urahisi zaidi.
6. Tumia mbinu hiyo na chunguz matokeo

Tafakuri

1. Ni mambo gani yaliyokusaidia katika kuwafahamu wanafunzi wenye matatizo katika kuelewa mada?
2. Kwa kuzingatia mbinu uliyotumia katika 5 + 6 (shughuli za kufanya). Ni mambo gani ungeyarekebisha katika ufundishaji wako wa baadaye?
3. Ujuzi ulioupata katika mada hii utakusaidiaje katika kutumia tungo za Kiswahili kwa Usahihi kwenye ufundishaji wako?

1.2 Kutumia tungo za Kiswahili kwa Usahihi.

Maudhui

Mpendwa mwalimu mwanafunzi, katika mada hii umejifunza:

- Maana ya tungo
- Aina za tungo za Kiswahili
- Miundo mbalimbali ya tungo za Kiswahili
- Namna ya kuitumia tungo katika mawasiliano

Sasa unapaswa kujikumbusha yafuatayo:-

Ujuzi

Baada ya kujifunza mada hii utaweza:

(a) Kueleza tungo za Kiswahili

(b) Kueleza miundo ya tungo mbalimbali za Kiswahili

(c) Kutumia tungo mbalimbali kwa usahihi katika mawasiliano.

Shughuli za Kufanya

a) Kwa kutumia mawazo yako mwenyewe eleza maana ya tungo.

b) Andaa zana utakazotumia kufundisha aina za tungo na miundo yake.

c) Tungo kishazi ni kubwa kuliko tungo kirai kwa kutumia mifano dhahiri. Eleza utakavyoongoza wanafunzi wako kuthibitisha kauli

Tafakuri:

1. Ni kwa vipi zana ulizotumia kufundishia aina za tungo zimeweza kufikisha ujumbe au maarifa uliyokusudia.

2. Ni maboresho gani muhimu yanahitajika katika maandalizi na matumizi ya zana katika ufundishaji wa mada husika?

1.3 Kuchambua sentensi za Kiswahili

Maudhui

Katika mada hii umejifunza:-

(i) Aina mbalimbali za sentensi na miundo yake.

(ii) Mbinu mbalimbali za uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili.

(iii) Kuchambua aina mbalimbali za sentensi.

Ujuzi

Baada ya kusoma mada hii utaweza:

(a) Kuainisha sentensi za Kiswahili.

(b) Kuchanganua sentensi za Kiswahili.

Shughuli za Kufanya

1) Ainisha aina kuu unazozifahamu za sentensi za Kiswahili.

2) Ukitumia mifano muafaka eleza mbinu utakazotumia katika ufundishaji wa:

(a) Sentensi (b) Sentensi Sahili (c) Sentensi ambatani

(d) Sentensi changamano.

3) Tumia mifano thabiti kuonyesha miundo mbalimbali ya sentensi sahihi kwa wanafunzi wako.

4) Kwa kutumia mbinu ya majadiliano, onyesha namna utakavyowaongoza wanafunzi kuchambua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi.

(a) Baba yangu alinunua machungwa jana usiku

(b) Abasi ni kijana mzuri

(c) Juma ni mrefu lakini Ally mfupi.

Tafakuri

1. Baada ya kumaliza mada hii ya uchambuzi wa sentensi unafikiri ni njia gani nyepesi ya kuchambua sentensi inayoweza kukusaidia wewe katika mtihani wako? Na ipi nyepesi inayoweza kueleweka kwa wanafunzi wako?

1.4 **Utata katika mawasiliano**

Maudhui

Katika mada hii umejifunza kwa kina yafuatayo:

(i) Maana ya utata katika mawasiliano.

(ii) Kubainisha chanzo cha utata.

(iii) Maana mbalimbali zinazojitokeza katika tungo tata.

(iv) Njia/mbinu za kuondoa utata katika tungo.

Ujuzi

Mwalimu mwanafunzi utaweza:

a) Kueleza dhana ya utata katika mawasiliano

b) Kufafanua chanzo cha utata katika mawasiliano

c) Kufafanua maana zinazojitokeza katika tungo tata

d) Kuonyesha njia mbali mbali za kuondoa utata katika tungo.

Kazi za Kufanya

1. Kwa kutumia mbinu ulizojifunza darasani/chuoni, elekeza wanafunzi wako kubainisha mambo yanayosababisha utata katika tungo na jinsi ya kuzuia utata huo.

Tafakuri

1. Ni kwa vipi umeweza kuwabainisha wanafunzi wenye uelewa mdogo?

2. Umewasaidiaje au unaweza vipi kusaidia kundi hili?

3. Ni changamoto zipi unaweza kukabiliana nazo katika kuwasaidia wanafunzi wenye uelewa mdogo?

4. Unazikabili vipi changamoto hizi?

1.5 Kutumia Kamusi

Maudhui

Katika mada hii umejifunza namna ya kutumia kamusi ya Kiswahili Sanifu kujifunza maneno mapya. Pia kwa njia ya mazoezi umebaini maana, aina na matumizi ya maneno kwa kutumia kamusi na mazoezi ya kupanga maneno Ki-kamusi. Pia umejifunza taarifa muhimu zilizoingizwa kwa kutumia Istilahi ya Kidahizo na Vibadala. Vilevile umejifunza utaratibu wa kuyagawa maneno katika makundi mbalimbali kulingana na kazi zianzofanywa na maneno hayo katika lugha pamoja na sifa zao nyingine za msingi.

Ujuzi

Baada ya kujifunza matumizi ya kamusi utaweza:-

- Kubaini maana, aina na matumizi ya maneno kwa kutumia kamusi.

Shughuli za Kufanya

1. Kwa kutumia kamusi waelekeze wanafunzi wako kutoa mifano dhahiri maana ya:-

(a) Kidahizo

(b) Vibadala vya Kidahizo.

2. Andaa somo la dakika 80 na ufundishe ugawaji wa maneno katika kategoria kwa kuonyesha bayana mbinu utakazotumia katika kuwasilisha mada hii/maarifa haya

Tafakuri

1. Bainisha changamoto uliyopata katika kutumia mbinu uliyo/zochagua.
2. Onyesha namna ambayo unaweza kukabili changamoto hii katika ufundishaji wa mada nyingine
3. Je matumizi ya kamusi yanakusaidiaje katika ufundishaji wa somo la Kiswahili?
4. Jiulize, je katika ufundishaji wako wa kila siku kuna ulazima wa kutumia kamusi?

MADA YA PILI:
MATAMSHI NA LAFUDHI YA KISWAHILI

2.1 Kutumia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili.

Maudhui

Katika mada hii umejifunza

i. Kutamka maneno ya Kiswahili kwa usahihi kwa kutumia jedwali la irabu na jedwali la konsonanti.
ii. Lafudhi mbalimbali za matamshi yanayotokana na athari za mazingira.
iii. Sauti za Kiswahili Sanifu na jinsi zinavyotamkwa na mahali pa kutamkia.
iv. Irabu za Kiswahili sanifu na Konsonanti za Kiswahili Sanifu na Viyeyusho vyake.
v. Maandishi ya kifonetiki.

Ujuzi

Baada ya kujifunza mada hii mwalimu utaweza:-

(a) Kutamka maneno ya Kiswahili kwa usahihi.
(b) Kutumia lafudhi sahihi ya Kiswahili katika mawasiliano.
(c) Kusahihisha makosa ya utamkaji wa maneno ya Kiswahili.

Shughuli za kufanya

1. Andaa somo na uonyeshe jinsi utakavyofundisha wanafunzi wako tofauti kutofautisha Lafudhi na Kiimbo, Irabu, konsonanti na kiyeyusho.

2. Andaa kazi itakayokusaidia kuwaelekeza wanafunzi kutofautisha maana ya sauti ghuna na zisizo ghuna (hafifu)
3. Onyesha jinsi utakavyofundisha wanafunzi wako kuandika maneno yafuatayo katika maandishi ya kifonetiki.
   (a) thamani (b) thelathini (c) ng'ombe (d) gharama.

4. Ikiwa mwanafunzi wako anashindwa kutamka na kutofautisha kati ya

(a) r na l

(b) **s na** □

(c) f na v

(d) s na z.

(a) Andaa somo uonyeshe utakavyomsaidia kutamka vizuri vitamkwa hivyo.

(b) Eleza sababu zinazosababisha kushindwa kutamka vizuri vitamkwa hivyo.

Tafakuri

1. Unaeleza vipi uwezo wako katika kufundisha mada ulizoelekezwa?

2. Ni mambo yapi ungependa kujifunza zaidi juu ya ufundishaji wa mada ulizofundisha?

MADA YA TATU:

FASIHI

2.2 Kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi

Maudhui

Mpendwa mwalimu mwanafunzi, katika mada hii umejifunza maana ya fasihi kwa kutumia mitazamo mbalimbali ya wanafasihi. Vilevile umejifunza umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi kazi mbalimbali za fasihi. Pia umeweza kuainisha mbinu/njia za kukusanyia kazi za fasihi na kubainisha ubora na udhaifu unaojitokeza katika uhifadhi wa kazi za fasihi.

Ujuzi

Baada ya kujifunza mada hii utaweza:

(a) Kueleza maana ya fasihi

(b) Kueleza umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

(c) Kuwezesha wanafunzi kuainisha njia mbalimbali za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

(d) Kueleza ubora na udhaifu wa mbinu/njia mbalimbali za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

Shughuli za kufanya

Ili kujijengea ujuzi wa hayo uliyojifunza fanya shughuli zifuatazo:-

1. Kwa kutumia mitazamo mbalimbali ya wanafasihi eleza jinsi utakavyofundisha wanafunzi wako kueleza maana ya fasihi. Pamoja na kubainisha tanzu zilizomo katika kila aina ya fasihi.

2. Andaa somo linalolenga kuwasaidia wanafunzi wako kuonyesha na kueleza njia/mbinu mbalimbali za kukusanyia na kuhifadhi kazi za fasihi.

Jipime

1. Kwa kutumia jedwali, jadili ubora na udhaifu wa njia/mbinu za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.
2. Eleza utakavyosimamia wanafunzi wako wa Kidato cha pili kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi simulizi zifuatazo:
   (i) vitendawili (ii) methali (iii) ngano.
3. Eleza utakavyotumia mkoba wako wa kazi kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi zilizoainishwa katika 2.
4. Je, katika kusoma mada hii umegundua matatizo gani katika ukusanyaji na uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi? Katika mazingira yako ya kazi?

2.3 Kutunga Kazi za Fasihi

Maudhui

Katika mada hii umejifunza kwa makini kwa kubainisha kanuni za utunzi wa kazi mbalimbali za fasihi simulizi na fasihi andishi. Vile vile umejifunza kutunga kazi mbalimbali za fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kutumia kanuni za Utungaji zilizoainishwa kwa kila utanzu wa fasihi. Sasa jishughulishe na haya yafuatayo:-

Ujuzi

Baada ya kujifunza mada hii utaweza:

(a) Kubaini kanuni za utunzi wa kazi mbalimbali za fasihi.

(b) Kutunga kazi mbalimbali za fasihi.

Shughuli za kufanya

1. Andaa somo la dakika 80 uoneshe jinsi utakavyowasaidia wanafunzi wako kubainisha kanuni za Utungaji wa fasihi simulizi (methali, vitendawili na hadithi).
   a) Ushairi
   b) Tamthiliya
   c) Hadithi (Riwaya)
2. Bainisha na tumia mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kuwawezesha wanafunzi kupenda kuandika.
3. Eleza ubora na udhaifu katika uwezeshaji wa ushairi, tamthiliya na hadithi (riwaya)

Tafakuri

1. Eleza jambo moja lililokuvutia au lililokupendeza wakati unawezesha kutunga kazi za fasihi.
2. Jambo hili lina maana gani katika ufundishaji na ujifunzaji darasani?

MADA YA NNE:
UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI

4.1 Misingi ya Uhakiki

Mpendwa mwalimu mwanafunzi, katika mada hii umejifunza maana ya uhakiki wa kazi za fasihi kwa kina. Pia umejifunza na kubaini misingi ya uhakiki kwa kutumia vigezo mbalimbali vya Uhakiki wa kazi za fasihi. Katika hatua hii unapaswa kujikumbusha ili kujenga uwezo wako Kitaaluma na Kitaalamu.

Ujuzi

Baada ya kumaliza mada hii utaweza:

kujijengea ujuzi ufuatao:-

(a) Kueleza kwa mifano dhana ya uhakiki

(b) Kubaini misingi ya uhakiki wa kazi za fasihi.

Shughuli za kufanya

1. Kwa kutumia mifano dhahiri wasaidie wanafunzi wako jinsi ya kubainisha vigezo vya uhakiki wa kazi za fasihi.
2. Fani na maudhui ndivyo vigezo vikubwa vya uhakiki wa kazi. Kwa kutumia mbinu ulizojifunza jadili jinsi utakavyofundisha wanafunzi wako wa Kidato cha tatu
3. Andaa somo la dakika 40 ukionyesha jinsi utakavyowafundisha wanafunzi wako wa Kidato cha tatu misingi ya uhakiki.

Tafakuri

1. Dhana ya kuwa “fani na maudhui” sawa na pande mbili za sarufi inajitoshelezaje katika uhakiki wa kazi za fasihi?
2. Vigezo vya uhakiki ulivyojifunza vimekusaidiaje katika uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi? Hii ina maana gani kwa mwalimu?

4.2 Kuhakiki Kazi za Fasihi

Maudhui

Mada hii ya uhakiki ni mada muhimu sana katika uwanja wa fasihi. Umejifunza katika nadharia na vitendo, natakiwa kujifunza zaidi kwa kupitia tahakiki mbalimbali na kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi.

Ujuzi

Baada ya kufanya mapitio utaweza:

Kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi kwa kufuata misingi ya uhakiki.

Shughuli za kufanya

1. Onesha jinsi utakavyofundisha wanafunzi wako kuhakiki kazi zifuatazo za fasihi:-

   Tamthiliya:-

   1. Ngoswe – Penzi kitovu cha Uzembe (Edwin Seimzaba)
   2. Mfalme Juha (Farouk M. Topan - Oxford University)

   Riwaya

   1. Kusadikika - Shabani Robert
   2. Watoto wa mama ntilie - Zainabu Mwanga.

   Ushairi.

   1. Mashairi ya Chekacheka – T. Mvungi
   2. Malenga Wapya - TAKILUKIZ
   4. Diwani ya Mloka - Charles Mloka.

Tafakuri

1. Kuna umuhimu gani kujifunza tamthiliya, riwaya, na ushairi?

2. Ni tabia gani mwalimu anapaswa kuwa nayo ili kuwawezesha wanafunzi kupata maana au maudhui kutokana na tamthiliya, riwaya na ushairi?

MADA YA TANO:
MAENDELEO YA KISWAHILI

Maudhui:

Mwalimu mwanafunzi, karibu kwenye sura hii ya maendeleo ya Kiswahili. Katika kujadili mada hii umejifunza nadharia zinazoeleza chanzo cha kuenea kwa Kiswahili, asili na chimbuko lake.

Ujuzi

Baada ya Kusoma na kuzingatia mada hii utaweza kueleza chimbuko la Kiswahili kwa kutumia ushahidi wa kihistoria. Utaweza pia kuonesha ushahidi wa kimsamiati na kimuundo kuhusu ubantu wa Kiswahili.

Shughuli za kufanya

Baada ya kusoma mada ya maendeleo ya Kiswahili na kuielewa inakubidi ufanye kazi zifuatazo:-

1. Andaa mifano mitano ukitumia Lugha yeyote ya kibantu ili kuthibitisha kuwa Kiswahili ni Kibantu. Onyesha waziwazi muundo wa silabi zinazojitokeza.
2. Fanya utafiti mdogo hapo shuleni na maeneo ya karibu na shule ili uweze kuwaeleza wanafunzi wako tofauti kati ya asili ya Kiswahili na Chimbuko la Kiswahili. Ni vema pia kuwatumia Wazee walio jirani na shule.
3. Fanya kazi ndogo ya kukusanya mifano ya Lugha za Kibantu kimuundo na kimsamiati na uziweke kwenye mkoba wako wa kazi.

Tafakuri

1. (a) Jipime mwenyewe kama unaweza kueleza asili na chimbuko la Kiswahili.
   (b) Jiulize kama una uwezo wa kuwasaidia wanafunzi wako kuonesha kwa kutumia mifano na ushahidi Ubantu wa Kiswahili.

5.1 Kukua na Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili katika Afrika Mashariki

Maudhui

Baada ya kusoma na kuzingatia mada ndogo ya asili ya lugha ya Kiswahili tunakukaribisha usome juu ya kukua na kuenea kwa lugha hii . Pia umejifunza vyombo mbalimbali vilivyohusika na ukuaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili hapa Tanzania.

Ujuzi

Baada ya kusoma na kuzingatia maelezo ya mada hii, soma vitabu vingine vinavyoeleza juu ya kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Baada ya hapo unaweza:-

(a) Kueleza dhana ya kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili na kueleza mambo yaliyosaidia ukuaji na ueneaji wake katika Afrika.

(b) Tunakutarajia uweze kueleza mafanikio na matatizo yanayovikumba vyombo vinavyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili katika Afrika Mashariki.

Shughuli za kufanya

Unatakiwa kufanya kazi mbili zifuatazo:

1. Kuwasaidia wanafunzi wako kuibua na kuorodhesha vyombo vilivyosaidia katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kuanzia Tanzania ilipata Uhuru.

2. Kuwasaidia wanafunzi wako kueleza kazi ya kila chombo.

3. Kuwasaidia wanafunzi kubaini matatizo na mafanikio yanayovikumba vyombo vinavyokuza na kueneza Kiswahili katika Afrika Mashariki?

Tafakuri

1. Jiulize kama unaweza kutoa maelezo ya kutosha kwa wanafunzi wako kuhusu kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

MADA YA SITA:
UFAHAMU

6.1 Ufahamu wa Kusikiliza

Baada ya kusoma na kujifunza mada hii ni matumaini yetu kuwa umebaini umuhimu wa Ufahamu wa kusikiliza kama mojawapo ya njia ya mawasiliano. Pia umejifunza umuhimu wa kusikiliza kwa makini ili kuelewa kiini kinachoongelewa. Vile vile umeweza kueleza maana ya maneno na misemo mbalimbali iliyotumika katika matini mbalimbali.

Ujuzi

Baada ya kusoma na kuzingatia mada hii utaweza:-

(a) Kueleza dhana ya ufahamu wa kusikiliza

(b) Kubaini mawazo makuu kutokana na habari uliyosikiliza

(c) Kujibu maswali yatokanayo na habari uliyosikiliza

(d) Kueleza maana za maneno na misemo kama ilivyotumika kwenye habari uliyosikiliza.

Shughuli za kufanya

1. Andaa habari kwa kuiandika. Waweza kuipata pia hii habari kutoka kwenye Redio au Luninga kisha ubaini mawazo makuu kutokana na habari hiyo.
2. Elekeza wanafunzi waisome habari hii kwa sauti na hakikisha kuwa wote wameisikia. Andaa maswali ambayo unaweza kumuuliza mwanafunzi ili uweze kufahamu kiasi chake cha ufahamu juu ya habari uliyosikiliza.

Tafakuri

1. Jipime mwenyewe kama unaweza kuwasaidia wanafunzi kusoma habari na kueleza maneno magumu na misemo ilivyotumika katika habari.
2. Orodhesha matatizo yanayoweza kujitokeza unapofundisha kusikiliza na kisha jiulize kama unaweza kuwasaidia wanafunzi kutatua matatizo hayo.

6.2 Ufahamu wa Kusoma

Maudhui

Mpendwa mwalimu mwanafunzi, baada ya kusoma mada ndogo hii umebaini aina za kusoma. Vilevile umebaini mawazo makuu na kueleza maana ya maneno na misemo iliyotumika katika matini mbalimbali uliyosoma.

Ujuzi

Baada ya kusoma na kuzingatia mada hii utaweza:-

a) Kueleza dhana ya ufahamu wa kusoma.
b) Kubaini mawazo makuu kutokana na habari uliyosoma.
c) Kujibu maswali kutokana na habari uliyosoma.
d) Kueleza maana na misemo kama ilivyotumiwa kwenye habari/matini uliyosoma.

Shughuli za kufanya

1. (a) Andaa habari ya kusoma kisha andaa maswali utakayowauliza wanafunzi wako kutokana na habari hiyo yanayohitilafiana katika ugumu wa fikra.

   (b) Katika habari hiyo hiyo andaa mazungumzo utakayoanza kabla ya kufundisha somo na baada ya kusoma na kuwauliza maswali ya mdomo

Tafakuri

1. Unadhani mazungumzo ya awali kabla ya kusoma kwa ufahamu yana faida kwako na kwa wanafunzi wako?
2. Jiulize kama unaweza kuwapa muda wanafunzi wataje makosa ya matamshi wenyewe. Je unafikiri kuwa unaweza kusaidia kurekebisha makosa yanayojitokeza mara kwa mara katika matamshi?

6.3 Ufupisho wa Habari

Maudhui

Baada ya kusoma kwa makini ufahamu wa kusikiliza na kusoma umebaini mambo muhimu ambayo yataweza kukusaidia katika kufupisha yale uliyoyasoma.

Pia umejifunza namna ya kuchambua mawazo makuu yatakayoweza kukusaidia wewe na wanafunzi wako kufupisha habari mtakazozisoma kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya habari.

Ujuzi

Baada ya kusoma na kuzingatia mada hii utaweza:

(a) Kueleza dhana ya ufupisho.

(b) Kufafanua misingi ya ufupisho wa habari.

(c) Kufupisha habari uliyosikiliza au uliyosoma kwa kuzingatia misingi ya kufupisha habari.

Shughuli za kufanya

1. Andaa kazi ya ufupisho kwa kidato cha pili kisha ifupishe kazi hiyo kwa ¾ kutoka habari ya asili kisha iweke kwenye mkoba wa kazi.
2. Andaa kazi ya ufupisho kwa kidato cha nne kisha ifupishe kazi hiyo kwa ⅓ kutoka habari ya asili kisha iweke kwenye mkoba wa kazi.
3. Tumia stadi ya ufupisho katika shughuli zako za kuandika shajara, kumbukumbu zako za somo darasani kisha andika ripoti ya ufundishaji wako kwa wiki nzima na iweke kazi hii kwenye mkoba wa kazi.

Tafakuri

1. Jiulize kama unaweza kueleza dhana ya ufupisho, misingi ya ufupisho na kama unaweza kufupisha habari uliyosoma au kusikiliza.

2. Je unaweza kutumia stadi ya ufupisho kwa kufupisha habari kuanzia fupi, rahisi hadi ndefu na ngumu?.

3. Je, unaweza kuandaa matini/habari ya ufupisho itakayokusaidia wewe kufundishia darasani?

MADA YA SABA:
UANDISHI

Mpendwa mwalimu mwanafunzi katika mada hii, umejifunza juu ya uandishi wa insha za aina mbalimbali. Pia umejifunza ufafanuzi wa aina mbalimbali za insha, mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha. Mwisho umejifunza pia kuandika insha kwa kuzingatia muundo wa insha na masuala mtambuko

Ujuzi

Mwalimu mwanafunzi utaweza:

(a) Kueleza dhana ya uandishi wa insha.

(b) Kufafanua aina za insha

(c) Kueleza mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha

(d) Kuandika insha kwa kuzingatia muundo wa insha na masuala mtambuko.

Shughuli za kufanya

Baada ya kusoma maelezo ya mada ndogo hiyo andaa matini za mifano ya insha za

(a) Kusimulia, kujieleza, kuhoji na kubuni. Unaweza kuwapa wanafunzi mfano wa insha ya masimulizi wakaandika na ziweke ubaoni au ukutani ili wazisome. Waonyeshe masuala mtambuko yanavyoweza kujitokeza na kujumuishwa katika kazi zao.

(b) Onyesha wanafunzi wako hatua kwa hatua miundo mbalimbali ya insha

Tafakuri

1. Jipime mwenyewe kama unaweza kuandika insha mbalimbali na kuingiza maswala mtambuko katika kazi zako.
2. Umewezaje kuwasaidia wanafunzi waingize maswala mtambuko kwenye kazi ya uandishi.

7.1 Uandishi wa Hotuba

Maudhui

Mpendwa mwalimu mwanafunzi, katika mada hii ndogo tunakukaribisha tena katika mambo muhimu uliyojifunza juu ya uandishi. Katika mada ndogo hii umejifunza:-

- Maana ya hotuba
- Mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba na
- Kuandika hutoba kwa kuzingatia mada za masuala anuai ya jamii.

Ujuzi

Mwalimu mwanafunzi utaweza:

(a) Kueleza maana ya hotuba.

(b) Kufafanua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba.

(c) Kuandika hotuba kwa kuzingatia mada za masuala anuai ya jamii.

Shughuli za kufanya

Baada ya kusoma mada ndogo hii na kuielewa. Andaa kazi zifuatazo:-

1. Kusanya hotuba mbalimbali zilizosomwa hapo shuleni, mfano Baraza la shule la wanafunzi, siku ya Wazazi, siku ya Mahafali na sikukuu mbalimbali. Angalia muundo wa hotuba hizo kuanzia utangulizi – kiini na hitimisho.

2. Husisha hotuba hizo na zile ulizotolea mifano darasani. Ni Mambo gani yaliyopungua na unajifunza nini zaidi. Soma ili upate ufahamu zaidi. Tumia shajara na mkoba wako wa kazi ili kutunza kazi zako.
3. Jifikirie kuwa wewe ni Mkuu wa Shule unayofundisha, na unatakiwa kuwa mgeni rasmi katika sherehe ya ufunguzi wa mradi mpya wa maji katika shule jirani. Fikiria kuwa umepewa nafasi ya kusoma risala ya kupokea mradi huo chini ya ufadhili wa nchi ya Canada. Andaa/andika risala itakayotumika katika tukio hilo.

Tafakuri

1. Je, unaweza kuwapa wanafunzi wako mwongozo wa kuandika hotuba nzuri?
2. Ni jambo gani jipya umejifunza katika uandishi wa hotuba? Tafsiri yake ni nini katika kufundisha na kujifunza?

MADA YA NANE:
SARUFI

Mpendwa mwalimu mwanafunzi, baada ya kusoma na kujifunza mada ya kwanza hadi ya saba tunakukaribisha katika mada ya Sarufi kwa ujumla.

Katika mada hii umejifunza

- Maana ya sarufi na tanzu zake.
- Pia umejifunza kwa kina miundo mbalimbali ya sarufi.
- Umejifunza pia ngeli za majina na muainisho wake.

Ujuzi

Mwalimu mwanafunzi mpaka wakati huu tunakutarajia wewe uweze;

1. Kuunda maneno mbalimbali ya Lugha ya Kiswahili.
2. Kuainisha ngeli za nomino kwa msingi wa maana.
3. Kutoa maelezo ya kutosha kwa wanafunzi wako kuhusu dhana ya uambishaji wa maneno na upatanisho wa kisarufi.

Shughuli za kufanya

Baada ya kusoma kwa undani vitabu vyenye mada hiyo hapo juu, tunakupa kazi zifuatazo.

(i) Fundisha mada ya uundaji wa maneno kwa wanafunzi wako. Wape kazi za kutosha ili waweze kuunda maneno mengi kwa kufuata kanuni ulizowaelekeza.

2. Katika idara yenu ya Kiswahili hapo shuleni jaribu

(ii) kuainisha ngeli kwa msingi wa maana. Baada ya kazi hiyo jaribu wewe mwenyewe na wanafunzi wako darasani mkitumia mifano mingi zaidi.

3. Weka kazi zote ulizofanya wewe, ulizofanya na wanafunzi na ulizofanya na walimu wenzako katika mkoba wako wa kazi.

Tafakuri

1. Jipime kama unaweza kuchunguza mizizi viambishi na mashina katika maumbo ya maneno ya Kiswahili.
2. Kwa kawaida Lugha nyingi za Ulimwengu zina mizizi funge na mizizi huru je unaweza kuwasaidia wanafunzi kutafuta mifano katika Lugha zao.
3. Jiulize kama unaweza kutoa mifano ya kutosha kuhusu
   - Viambishi vya njeo
   - Viambishi vya unyambulishi katika vitenzi
   - Viambishi vya nafsi
   - Viambishi vya hali
   - Viambishi virejeshi
   - Viambishi vya Nomino
   - Viambishi kanushi.

ORODHA YA VITABU

1. Kapinga, M.C. (1983), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili, TUKI, Dar es Salaam.*
2. Nkwera, F.V. (1979) *Sarufi na Fasihi*. *Sekondari na Vyuo, T.P.H. Dar es Salaam.*
3. Senkoro, F.E.M.K. (1998) Ushairi. *Nadharia na Tahakiki, DUP, Dar es Salaam.*
4. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988), *Kiswahili Sekodnari TUMI, Dar es Salaam*.
5. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1992), *Kiswahili Vyuoni, KIUTA – Dar es Salaam*.
6. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1999), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na vyuo, TUKI, Dar es Salaam.*
7. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, (1999), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na vyuo, TUKI Dar es Salaam.*
8. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (1996), *Fashi ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.*
9. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (1996), *Fasiji ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.*
10. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Oxford University Press East Africa Ltd., Kenya.*
11. Mulokozi, M.M. na Mung'ong'o, C.G. (Wah) 1993 Fasihi, *Uandishi na Uchapishaji KWVITA/DUP, Dar es Salaam.*
12. Topan F. (mh) 1977 *Uchambuzi wa maandishi ya Kiswahili 2, OUP Nairobi*.
13. TUKI 1983 Makala ya semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 3: *Fasihi. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.*